


HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.



TAARIFA KWA UMMA.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inakusudia kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha mbolea kitakachotumia malighafi ya taka kutoka katika masoko (composting plant for Organic Market waste) kitakacho jengwa eneo la Mabwepande Kata ya Mabwepande wakati wowote kuanzia sasa.

Hayo yamesemwa leo na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe Benjamini Kawe Sitta Katika Mkutano wa Wadau katika ukumbi wa Manispaa ya Kinondoni ulioandaliliwa kama moja ya njia sahihi za kutoa elimu kwa umma juu ya mradi huo na kuufanya kuwa fursa ya pekee kwao mara utakapokamilika.

Mradi huu unafadhiliwa na Jiji la Hamburg la ujerumanu kutokana na Uhusiano mzuri uliopo kati ya Jiji la Hamburg na Jiji la Dar es Salaam ambapo katika makubaliano yaliyofikiwa ,Jiji la Hamburg litagharamia ujenzi wa mradi na kuendesha kwa muda wa mwaka mmoja ambapo katika muda huo itawajengea uwezo wataalamu wa Manispaa ya Kinondoni katika uendeshaji wa Kiwanda hicho.

Mradi huu wa Kiwanda unatarajia kugharimu kiasi cha **Euro 1,547,277** sawa na **Bilioni 4.1** za kitanzania ambapo kati ya hizo Jiji la Hamburg litatoa

Euro 1,047,787 sawa **Tshs 2,789,649,064.54** na **Euro 499,490** sawa na

Tshs 1,329, 852, 165.8 zitatorewa na Serikali ya Ujerumanu(German Federation Government)ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetoe eneo la